

»DAWA ASILI YA KUKU KWA BEI NAFUU«

Ndege huathiriwa na magonjwa kadhaa, yale ya kawaida ni mharo, homa ya matumbo, kideri, ndui ya kuku, na upungufu wa lishe. Kupitia hatua asili za kikaboni magonjwa yanaweza kudhibitiwa.

Magonjwa haya yanatambuliwa na uzalishaji duni wa mayai, ulaji mdogo wa chakula, kifo na makamasi kutoka puanī.

Daima ni muhimu kusafisha vyombo vya maji kwa sabuni, na kuwapa ndege chakula cha usawa.

Iwapo unatibu minyoo, wape ndege dondo la komamanga, na utomvi wa papai kwa siku 5 mfululizo.

Maganda ya mayai yanapaswa kuchemshwa kabla ya kuponda na kuongezwa kwenye malisho ili kudhibiti ndege dhidi ya ulaji wa mayai.

Udhibiti wa kikaboni

Kwanza, safisha vyumba vya kuku kila siku ili kudhibiti magonjwa.

Daima wape ndege maji safi ya kutosha, kwa kuongeza potasiamu pamanganeti kwenye maji hayo ili kudumisha afya ya ndege.

Kisha ongeza vitunguu saumu na vitunguu kwenye malisho mara moja kwa wiki ili kuzuia maambukizo, na walishé ndege kwenye majani machungu ya mitishamba mara moja kwa mwezi.

Tibu minyoo kwa kuwapa ndege dondo ya komamanga, na vijiko 5 vya utomvi wa papai uliochanganywa na maji.

Liche ya hayo, changanya karanga za siagi zilizokatwa katika vyakula vya mifugo mara moja kwa mwezi ili zifanye kama dawa ya minyoo.

Daima ongeza maganda yiliyochemshwa katika vyakula nya kuku ili kutoa kalsiamu kwa ajili ya uundaji wa ganda la yai lenye nguvu.

Pili, ongeza chokaa, na unga wa ngano kwenye vyakula vyakula kuku ili kuzuia upungufu wa kalsiamu na kuhimiza uzalishaji wa mayai bora.

Mwishowe, tumia majani ya mikaratusi, nyasi limao, rose Mary, mtukutu kwenye nyumba za ndege ili kuzuia vimelea.